TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MKUKUTA 2009/10

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

MDAHALO **KUHUSU** SERA ZA KITAIFA

TAREHE 2- 8 DESEMBA BLUE PEARL HOTELI

UBUNGO PLAZA

YALIYOMO

- Utangulizi
- Utekelezaji na Mafanikio
- Changamoto

1. Utangulizi

- MKUKUTA ni mkakati wa Kitaifa wa muda wa kati (miaka 5) katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) na Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015;
- MKUKUTA I umetekelezwa kwa miaka 5 (2005/06-2009/10, hivyo Ripoti ya 2009/10 inaelezea mafanikio ya utekelezaji katika kipindi miaka 5;
- Kila mwaka Ripoti za utekelezaji zinazoonyesha mafanikio, changamoto, mambo tuliojifunza na hatua za kuchukua kwa uboreshaji, zimekuwa zikiandaliwa na kuwasilishwa kwenye midahalo ya kitaifa inayohusu sera kama huu;
- Ripoti hii kila mwaka hutoa mchango katika maandalizi ya Mwongozo wa mipango na bajeti kwa mwaka unaofuata.

Utangulizi.....Inaendelea

- Katika kipindi cha mwaka 2009, Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali ilifanya mapitio ya MKUKUTA I kwa ajili ya Maandalizi ya MKUKUTA II;
- Mapitio haya yalipitia hatua mbalimbali ikiwemo:
  i. Tafiti katika maeneo ya ukuaji uchumi, kilimo, mazingira, raslimali watu katika sekta ya afya, maboresho, namna ya kuboresha mfumo wa kugharamia utekelezaji, n.k.,
  ii. Mijadala ya kuhusu matokeo ya tafiti ikishirikisha wadau na makundi yote nchini,
  iii. Mijadala ya rasimu ya MKUKUTA II (Januari-Juni 2010),
- Matokeo ya Mapitio pamoja na mijadala ya wadau yaliainisha mikakati na hatua muhimu za kuimarisha utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya pili.

2. Utekelezaji na Mafanikio

a) **Nguzo ya I:Kukuza Uchumi na kupunguza Umaskini wa Kipato**

i. **Kuhakikisha Usimamizi Mzuri wa Uchumi:**

- Mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 5 mwaka 2005 hadi asilimia 12.1 mwaka 2009, ongezeko limetokana na athari za kupanda kwa bei za mafuta na chakula katika soko la dunia, na athari za msukosuko wa uchumi duniani;
- Ukusanyaji wa mapato umeongezeka, kutoka asilimia 12 mwaka 2005/06 na kufikia asilimia 16 mwaka 2009/10,
- Hadi Aprili 2010, ajira mpya 1,313,561 zilipatikana nje ya sekta ya kilimo, ambapo sekta binafsi ilizalisha ajira 1,185,387, na sekta ya umma ajira 128,174.

....Inaendelea

ii. **Ukuaji wa uchumi endelevu wenye kunufaisha watu wengi**

- Uchumi umeendelea kuimarika, na kukua kwa wastani wa asilimia 7, tangu mwaka 2005, sambamba na malengo ya MKUKUTA ya ukuaji wa asilimia 6-8 kwa mwaka.

iii. **Uhakika wa Chakula katika Ngazi ya Kaya, Mijini na Vijijini**

- Japakuwa hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula iliathiriwa zaidi na hali mbaya ya hewa, kwa ujumla tangu mwaka 2005, kumekuwa na utoshelevu wa chakula nchini.

....Inaendelea

iv. **Kupunguza Umaskini wa Kipato**

- Hali ya Umaskini hupimwa kwa kuangalia viashiria vya umaskini wa kipato na umaskini usio wa kipato
- Umaskini wa kipato umepungua kwa kiwango cha asilimia 2.1, kutoka asilimia 35.7 mwaka 2001 hadi asilimia 33.6 mwaka 2007. Kiwango hiki ni pungufu ya ongezeko la idadi ya watu la asilimia 2.9 kwa mwaka.
- Umaskini wa chakula ulipungua kutoka asilimia 18.7 mwaka 2001 hadi asilimia 16.6 mwaka 2007

Mwenendo wa Umaskini wa Kipato: HBS 1991, 2001, na 2007

Year	Dar es Salaam	Other Urban areas	Rural areas	Tanzania
1991/92	28.1	28.7	40.8	38.6
2000/01	17.6	25.8	38.7	35.7
2006/07	16.4	24.1	37.6	33.6

....Inaendelea

v. **Utoaji wa nishati ya uhakika na nafuu:**

- Serikali imeendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ndogo ya umeme ili kuwezesha wazalishaji binafsi wa umeme kufanya biashara katika sekta hii, na wakati huo huo kupanua wigo wa upatikanaji wa umeme.

…. Inaendelea

b. **Nguzo ya II: Ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii:**

i. Kwa ujumla mafanikio ni makubwa, utekelezaji katika kuboresha huduma za elimu na afya zimefanikiwa na kuifanya Tanzania kupanda katika upimaji wa maendeleo ya binadamu yaani “Human Development Index” kutoka nafasi ya 163 mwaka 2000 hadi kushika nafasi ya 151 mwaka 2009, hivyo kutoka kwenye kundi la nchi za chini na kuingia katika nchi za kati.

ii. Katika Mkutano wa viongozi wa Nchi kuhusu Maendeleo ya Malengo ya Milenia (MDGs Summit) uliofanyika New York mwezi Septemba 2010, Tanzania ilizawadiwa cheti cha kufanya vizuri kwenye uandikishwaji wa wanafunzi elimu ya msingi, ambayo imeonekana maendeleo ni mazuri na uwezekano wa kufikia malengo ya MDGs 2015 ni mkubwa.

....Inaendelea

i. **Elimu bora ya Awali, Msingi, Sekondari, ufundi na Elimu ya Juu kwa wasichana na wavulana:**
   - Kama Ripoti 2009/10 ilivyoonesha, mafanikio yameonekana katika ngazi zote za elimu kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari, elimu ya ufundi na elimu ya juu.

ii. **Afya na ustawi wa watoto na wanawake**
   - Afya za watoto na mama wajawazito zimeboreka, hii ni kwa mujibu wa utafiti wa 2009/10 (DHS) ambapo vifo vimepungua, taarifa zaidi kwenye mada husika.
   - Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua toka watoto 112 (2004/05) hadi 91 (2009/10) kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai.

....Inaendelea

- Idadi ya vifo vya watoto wachanga vilevile vimepungua kutoka watoto 68 (2004/05), 58 (2007/08) hadi 51 (2009/10) kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai;
- Aidha, vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi vilipungua kutoka 578 (2004/05) 454 (2009/10) kwa kila kina mama waliojifungua watoto hai;
- Huduma ya chanjo imepanuka zaidi kutoka watoto 1,249,388 mwaka 2005 hadi watoto 1,356,421 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 8.0;
- Mikakati ya kudhibiti utapiamlo, malaria, kifua kikuu, UKIMWI na vurusi vya UKIMWI imeendelea kutekelezwa.

....Inaendelea

iii. **Upatikanaji wa maji safi na salama na nafuu, usafi wa mazingira na makazi bora**

- Bunge lilipitisha sheria ya Usimamizi wa Maji Namba 11 ya mwaka 2009 na Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Namba 12 ya mwaka 2009;
- Usambazaji wa huduma ya maji umeongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 2005 hadi asilimia 58.7 mwaka 2009;
- Mwenendo wa upotevu wa maji umepungua toka asilimia 42 mwaka 2006 hadi asilimia 35 mwaka 2010;
- Katika jiji la Dar es Salaam; DAWASA imeboresha ukusanyaji wake wa mapato kwa zaidi ya asilimia 90 ikilinganishwa na mwaka jana, na imeongeza huduma ya usambazaji maji toka asilimia 50 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 68 mwaka 2009.

....Inaendelea

iv. **Kinga ya Jamii na Makundi maalum**

- Mfumo wa kinga ya jamii umeandaliwa na uko katika hatua ya kupitishwa na BLM;
- Mikakati mbalimbali imetekelezwa, Mfano, mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF) tangu mwaka 2005 mpaka mwezi Mei 2010, jumla ya miradi 9,012 iliainishwa kwenye halmashauri;
- Miongoni mwa miradi hiyo, miradi 7,546 ilipatiwa jumla ya Shilingi bilioni 156, na Jumla ya miradi 4,078 imekamilika na kukabidhiwa kwa jamii;
- Aidha, jumla ya vikundi 1,720 vyenye wanachama 21,712 vilianzishwa, ambapo asilimia 58 ya vikundi hivyo vilipatiwa vifaa kwa ajili ya kuweka na kukopa sambamba na kupatiwa ujuzi wa uendeshaji.

....Inaendelea

c. **Nguzo ya III: Utawala Bora na Uwajibikaji**

i. **Uwiano katika ugawaji wa rasilimali za umma na udhibiti wa rushwa**

- Hatua mbalimbali zimechukuliwa kuboresha ukusanyaji wa mapato, ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kurekebisha sheria na kanuni mbalimbali, mfano sera ya madini;
- Rasilimali katika Serikali za mitaa zimeongezeka.

....Inaendelea

ii. **Kuboresha Mifumo ya huduma za umma**

- Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya utawala katika taasisi zote za umma ikiwa ni pamoja na kuboresha utumishi wa umma kwa kuanzisha mikataba ya wateja, maboresho katika sekta ya sheria, kutangaza katika vyombo vya habari fedha za bajeti katika Serikali za Mitaa, kuimarisha kamati za kusimamia huduma za jamii kama vile kamati za maji n.k.;
- Kupeleka madaraka karibu na wananchi kwa kuimarisha Serikali za mitaa.

iii. **Haki za Binadamu na makundi tete zinalindwa na kuendelezwa katika Mfumo wa Sheria**

- Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria zimeleta mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na;
  - kupungua kwa ucheleweshwaji wa kesi mahakamani,
  - kufanyika kwa kina kwa uchambuzi na mchakato wa mashitaka,
  - kuboresha elimu ya wataalam wanao wahudumia watoto wanaokinzana na sheria.

....Inaendelea

- Serikali imeendeleza adhima yake ya kuridhia mikataba mbali mbali ya kimataifa juu ya haki za binadamu;
- Kati ya mwaka 2005 hadi 2010, Serikali ilitoa mafunzo kwa maafisa wa polisi 12,536 kuhusu masuala ya utawala bora na haki za binadamu.;
- Mrundikano wa wafungwa umeendelea kupungua;
- Jitihada za kudhibiti biashara haramu zinaendelea kuboreka.

Inaendelea

iv. **Kukuza Utamaduni wa Taifa:**

- Kumekuwa na Maendeleo mazuri katika suala la utamaduni na utambulisho wa taifa mfano:
  - **Vyombo vya Habari**: Serikali imeendelea kuanzisha na kutekeleza sera ambazo zitahakikisha kuna uhuru wa vyombo vya Habari. Hadi kufikia Mei 2010 Serikali ilikuwa imesajili Magazeti na Majarida 710, vituo vya redio 59, na vya Luninga 28.
  - **Utamaduni** na urithi wa kihistoria, Kiswahili kama utambulisho wa Taifa na Uzalendo na Kujiamini kimeendelea kukua kwa kuongeza misamiati mbalimbali kukidhi mahitaji

3. Changamoto

- Pamoja na mafanikio, changamoto zipo, baadhi ni:
  - Kuimarisha uratibu katika utekelezaji;
  - Kuimarisha ushirikiano wa sekta za uchumi katika kupanga na kutekeleza mikakati;
  - Kuboresha uzalishaji katika sekta ya kilimo na kusindika mazao na kuongeza thamani ya bidhaa zinazo zalishwa nchini;
  - Kuboresha upatikanaji wa huduma za mikopo nafuu kwa wakulima na wawekezaji wadogo;
  - Kuboresha sekta ya miundombinu ikiwemo barabara za vijijini, reli na bandari, na upatikanaji wa nishati ya umeme.

Changamoto....Inaendelea

- Kuboresha kiwango cha ubora wa huduma za jamii;- elimu, afya na maji;
- Kuongeza idadi ya raslimali watu katika sekta zote za uchumi;
- Kuimarisha mifumo ya usimamizi raslimali za umma;
- Kuimarisha mifumo ya ushirikishwaji wadau katika kupanga mipango ya maendeleo;

Changamoto hizi zimeweka misingi ya maandalizi ya vipaumbele vya MKUKUTA II (2010-2015).

<u>MWISHO</u>

Asanteni kwa kunisikiliza, A. Mwasha, DPEE